Elimu na Malezi

We speak your language ☎ 13 1202

Education and training – Swahili

Hii habari ni kwa wateja walioingia ndani ya Australia na visa ya ukimbizi

Hii habari itakwambia jinsi Centrelink inaweza kukusaidia kuendeleza elimu yako. Kwa watu wengine Centrelink yaweza kuwasaidia na gharama ya kuishi wanaposoma, gharama ya kozi au mtihani.

Kwa nini kusoma?

Kupata elimu nzuri ni muhimu. Kuwa na elimu na maarifa zaidi inaweza kuongezea imani na uwezo wako na pia kuongezea bahati yako ya kupata kazi.

Kama nimeacha shule Centrelink inaweza kunisaidia vipi?

Kama una miaka 13 hadi 19 na umeacha au unafikiria kuacha shule mbele ya kumaliza darasa la 12. Tunaweza kukurejea kwa mpango wa **Youth Pathways (njia ya Vijana)**. Wanaweza kukupa msaada na shauri ni nini unayoweza kufanya baadaye.

Kuna mazimio zingine zinayoweza kunisaidia?

Kama una miaka ya 13 mpaka 19 na hujaenda shule kwa muda kuzidi Mwezi 3 unaweza kujaribu azimio la **Connections (viungo)**. Wanaweza kukupa msaada na kushughulika na matatizo ya kibinafsi na kukusaidia kujihisi na imani zaidi.

Career Information Centres

Kwa Career Information Centres (Vituo vya habari kuhusu Shughuli) unaweza kupokea habari juu ya:

- Ungamo tofauti
- Kurudi kwa masomo
- Uchaguzi wa wito
- kozi za chuo kikuu na TAFE
- Soko la kibarua ya Australia
- Jinsi ya kupata kazi na kutengeneza resume.

Hii ni huduma ya bure. Mtu yeyote anaweza kuitumia Career Information Centres sio makastoma wa Centrelink peke yao.

Usaidizi kwa gharama zingine zinazoambatana na masomo yako

Kama una miaka 16 -24 na unasoma saa zote unaweza kulipwa malipo inyoitwa inayoitwa **Youth Allowance (Malipo ya vijana).**

Ikiwa, kama una miaka inayozidi 25 na unasoma saa zote au unafanya uanafunzi kiwandani saa zote unaweza kulipwa malipo inayoitwa **Austudy**.

Kama wewe ni mwanafunzi wa chuo kikuu, kuna malipo inayoitwa **Fares Allowance (usadizi wa nauli)** kukusaidia kulipa malipo ya usafiri kutoka nyumbani mwako na mahali unaposomea.

Uanafunzi Kiwandani

The Australian Apprenticeship Access Programme (Programu ya uanafunzi kiwandani ya Australia) itakusaidia upate uanafunzi. Hii itakusaidia kusoma ufundi na kuwa na ujuzi.

Group Training in the Trades Program (Kundi la malezi katika utaratibu la ufunzi wa ufundi) yaweza kukupa malezi unayohitaji kupata ili uanze uanafunzi kiwandani. unaweza kuanza uanafunzi kiwandani ukiwa bado unasoma shule mwaka 11 ao 12.

Kuendeleza ujuzi wako wa kingereza na na elimu ya hesabu

Language Literacy and Numeracy Programme - LLNP (Utaratibu wa Lugha, Ujuzi na Kihesabu) inaweza kukusaidia.

Maisha yatakuwa rahisi kama una ujuzi nzuri wa kingereza na hesabu, hivyo unaweza kusoma ratiba ya basi au treni. Unaweza kuandikia watu barua na kuandika maombi ya kazi.

Centrelink itakulipa unaposoma mpaka lini?

Centrelink itakulipa tu unaposoma kozi fulani kwenyi shule zinazokubaliwa. Hatutaendelea kukulipa ukiendelea kusoma mda mrefu ikiwa tunafikiri uko tayari kupata kazi.

Kama umemaliza masomo ya diploma ao digrii kwa chuo kikuu myezi 12 au zaidi Centrelink itakusaidia tu kulipia kusoma kozi iliyo kwa madaraka tofauti.

Kuna mtihani wa uchumaji kwa malipo za Austudy au Youth Allowance kuna mtihani wa mshahara kuhusu malipo ya Austudy au Youth Allowance (Malipo ya Vijana) ambayo inaweza geuza malipo tutakayo kulipa.

Lazima uasiliane na Centrelink kwa habari zaidi na kuhusu kozi zinazoruhusiwa na shirika zinazoruhusiwa, na kwa habari zaidi kuhusu malipo yanayowezekana kulipwa unaposoma.

Kupata wasifu Wako wa Ngambo kukubaliwa ndani ya Australia

Kama umesomea ngambo na umepata wasifu fulani ya ufundi au ubingwa, **Australian Education International** (zamani inayojulikana kama NOOSR – the National Office of Overseas Skills Recognition (Ofisi ya kitaifa ya Ukubaliaji wa Sifa wa Ngambo) Inaweza kukusaidia sifa yako ya ngambo ukubaliwe.

Australian Education International (Elimu ya Australia ya Mataifa) inaweza pia kukusaidia kulipa malipo maalum kama malipo za mtihani inayotakikana ili ukubaliwe (ili ukubaliwe kufanya kazi inchini Australia). Huu usaidizi ya kifedha hujulikana kama **Assessment Subsidy for Overseas Trained Australian Residents (Msaada wa kifedha kwa wenyeji wa Australia walioelimiwa ngambo).** Sio kila mtu anayeweza kupata huu usaidizi kwa hiyo wasiliana na Centrelink kama una haki ya kulipata.

Karatasi wa baina kwa mandamano hii kwa wakimbizi wapya katika Australia:

- *Fedha Ya kukusaidia*—ni kwa nini tunakulipa na pesa inatakikana kutumiwa vipi
- *Usaidizi na Gharama*—Ibada zinazoweza kukusaidia kuokoa pesa
- *Usaidizi katika lugha yako*—Kuongea na Centrelink katika lugha yako
- *Usaidizi wa kibinafsi*—mtu wa kuongea na Centrelink na kukupa msaada
- *Haki na sharti zako*—Vitu unavyostahili kutuambia na ufanye, na nini unaweza kutazamia kutoka Centrelink
- *Kusoma Kingereza*—machaguo la kusoma kingereza nchini Australia
- *Elimu na Malezi*—Kuendeleza elimu, ujuzi na sifa zako

Kumbuka: Hizi habari inweza kupatikana kwa mwandiko na kwa vifaa vya kusikiza.

Kuongea na Centrelink katika Kiswahili, piga simu **13 1202***.
Maelezo katika Kiswahili yanaweza kupatikana kwa mtandao **www.centrelink.gov.au**

** Malipo ya kupiga simu kutoka simu yako ya nyumbani kwa simu za Centrelink namba "13" huwa tofauti kutegemea na mtoaji wa huduma ya simu yako. Simu kwa namba "1800" kutoka simu yako ya nyumbani ni bure hazilipishwi. Simu kutoka kwa simu ya hadharani na simu ya mkono hulipishwa bei ya juu.*